

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO



TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI
(THE INSTITUTE OF CONSTRUCTION TECHNOLOGY- ICoT)

TANGAZO

NAFASI ZA MASOMO KWA MWAKA WA MASOMO 2020/21

1. UTANGULIZI

Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) imeanzisha Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (*Institute of Construction Technology – ICoT*) iliyosajiliwa na NACTE kwa namba ya usajili **REG/SAT/035P**. Taasisi hii imeanzishwa kwa kuunganisha kilichokuwa chuo cha Ujenzi Morogoro (MWTI) na Chuo cha Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (ATTI) Mbeya vilivyokuwepo chini ya Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi). Makao Makuu ya Taasisi hii (Main Campus) yatakuwa Morogoro kilipokuwa Chuo cha Ujenzi (MWTI) na kutakuwa na Tawi (Campus) ya Mbeya kilipokuwa Chuo cha ATTI – Mbeya.

2. LENGU LA KUENZISHA TAASISI

Uanzishwaji wa Taasisi hii unaendana na malengo ya Serikali ya kufikia Uchumi wa Kati ifikapo mwaka 2025 na nchi ya uchumi wa viwanda ambapo Sekta ya Ujenzi ni mdau muhimu katika kusaidia nchi kufikia malengo hayo. Hivyo, ili kufikia malengo hayo Tanzania inatakiwa kuwa na wataalam wa kutosha katika Sekta ya ujenzi katika ngazi za chini (artisans), kati (technicians) na wa juu (engineers). Aidha, hatua za Serikali zinaenda sambamba na malengo ya Sera ya Ujenzi ya mwaka 2003 inayosisitiza na kuhakikisha kuwa wataalam waliopo wanajengewa uwezo wa kitaalam katika ufundi ili kuendana na hali ya sasa ya ukuaji wa sayansi na teknolojia. Hii itawezesha kukabiliana na ushindani na kupata thamani halisi ya fedha zinazopelekwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

3. KOZI ZINAZOTOLEWA

NA.	AINA YA MAFUNZO	SIFA ZA KUJIUNGA	MUDA WA MAFUNZO
1	Basic Technician Certificate - NTA Level 4 - Civil Engineering	Mwombaji awe na ufaulu unaoanzia alama "D" katika masomo ya Hisabati, Fizikia au <i>Engineering Science</i> ,	Mwaka mmoja (1)
2	Basic Technician Certificate - NTA Level 4 - Electrical Engineering	Kiingereza na somo lingine moja isipokuwa masomo ya dini kwa ngazi ya kidato cha nne au Cheti cha Ufundi Stadi (VETA) Level 3	
3	Basic Technician Certificate - NTA Level 4 - Mechanical Engineering	kikiambatana na ufaulu wa kuanzia alama "D" katika masomo mawili kwa ngazi ya kidato cha nne.	

4. ADA

Ada zetu ni nafuu na zitalipwa kwa awamu moja au mbili kulingana na uwezo wa mwanafunzi. Pia, Chuo kinatoa huduma za hostel kwa wanafunzi watakao wahi. Maelezo mengine yanapatikana katika masharti ya udahili yanayopatikana Chuoni au kupitia mawasiliano yaliyotolewa hapo juu.

5. MAELEZO YA KUJIUNGA NA CHUO

- Waombaji wote wenye sifa wanapaswa kuwasilisha maombi yao kwa:

Mkuu wa Chuo,
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT),
S.L.P. 963,
MOROGORO.
Tel. +255 23 2614098
Fax +255 23 2935227

- Fomu za kujiunga na Chuo zinapatikana kwa Mkuu wa Chuo, Morogoro simu +255 23 2614098/ 0685541188, ATTI - Mbeya simu namba 0784500738 na Makao Makuu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) - Dodoma simu namba +255 26 2324455 / 0713815110 / 0712607291. Fomu hizi pia zinapatikana katika Tovuti ya Wizara ambayo ni www.mwtc.go.tz.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20 Novemba, 2020.

Wahi ili upate nafasi katika chuo chetu ambacho ni miongoni mwa vyuo vichache vya Serikali ya Tanzania vinavyofundisha fani hizi kwa vitendo zaidi.